

Majaribio ya matumizi ya DE yenye kuwahusisha wakulima yanafanyika kwenye kanda 3 za Kilimo (AEZ) katika Mikoa ya Shinyanga, Dodoma na Manyara. Majaribio haya yanapima uwezo wa DE kudhibiti wadudu wa hifadhi katika mazingira tofauti ya hali ya hewa katika mazao mbalimbali, hususan mahindi, mtama na maharagwe.

Majaribio yanahusisha madawa kadhaa kwa viwango tofauti kama ifuatavyo.

- D.E aina ya Protect it na Dryacide kwa viwango viwili vya gramu 100 za DE kwa kilo 100 za zao na gram 250 za D.E kwa kilo 100 za zao kwa kila aina ya D.E.
- Protect it iliyochanganywa na Permethrin kwa uwiano wa gramu 100 kwa kilo 100 (Protect it ) na milligram 200 kwa kilo 100 (permethrin).
- Actellic Super dust kiwango cha gramu 90 kwa kilo 90 za zao
- Dawa za kienyeji ambazo zinatofautiana sehemu na sehemu, ikiwa ni pamoja na majivu, pumba ya mpunga, majivu ya samadi na majani ya mimea ya aina mbalimbali. Nyingi ya madawa ya kienyeji hutwa bila kupepetwa zao husika.
- Hifadhi bila chochote. Hii ni kuweza kulinganisha matokeo ya matumizi ya madawa na bila matumizi ya madawa.

Wataalamu wa mradi wamekuwa wanatembelea sehemu za majaribio kila baada ya wiki 8 kwa muda wa miezi 10 ili kuchukua sampuli na kuzichunguza kwenye, maabara. Uchunguzi huo unahusisha kiwango cha uharibifu wa wadudu, idadi ya wadudu waliopo walio hai na waliokufa.

Wakukulima kwenye maeneo ya majaribio wanapata fursa ya kuona maendeleo ya majaribio haya. Hata hivyo walifanya tathmini wenyewe ya mafanikio ya majaribio haya kwa kulinganisha kiwango cha udhibiti wa wadudu kwa kila aina ya dawa. Taarifa hii ni matokeo ya tathmini hiyo na umuhimu wake.

## **2. Maandalizi ya Tathmini**

Kabla ya kufanyika tathmini, wataalamu walifanya majadiliano na viongozi kwenye maeneo haya, ikiwa ni pamoja na Maafisa watendaji wa vijiji, Mabwana shamba, Mwenyekiti wa kijiji n.k na kupanga jinsi ya

kuhusisha wakulima katika kufanya tathmini ya majaribio ya hifadhi mazao yanayojumuisha matumizi ya D.E.

Kwa kuzinatia kwamba wakulima wamegawanyika kwenye makundi yenye sifa tofauti na kwamba makundi hayo yanaweza kuwa na mtizamo tofauti katika tathmini kulingana na sifa za kundi hilo iliamuliwa kuhusisha sifa ya (kipato) uwezo.

Aidha wakulima waligawanywa kwenye makundi matatu ya sifa hiyo, yaani kundi la wenye uwezo, kundi la kati na wenye uwezo mdogo (masikini).